5455

# MAFUNZO YA SALA

KWA MUJIBU WA FATWA ZA

TABATABAI AL-HAKEEM, MOHAMMAD SAEED

Kimetafsiriwa na:

Al-Akh: Ramadhani Z. Ndiholeye

Kimehaririwa na: Khalifa M. Mlili

DARUL-HILAL

www.ketab.ir

سر شناسه: طباطبائی حکیم، محمد سعید، ۱۹۳۵م- Tabatabai Al-Hakeem , Mohammad Saeed

عنوان قرار دادی: تعلیم الصلاة/ سواحلي/ / عنوان: MAFUNZO YA SALA

تکرار نام پدید آور: محمد سعید طباطبائی حکیم/ ترجمه: Ramadhani Z Ndiholeye :

قم، دار الهلال، ۱۴۳۶هـ.ق= ۱۳۹۴هـ. ش= ۲۰۱۵م

۵۶ ص . چاپ اول، مصور ، وضعیت فهرست نویسی: فیپا / یادداشت: زبان : سواحلي.

شابك: ISBN: 978-600-6992-27-3

موضوع: ۱ ـ نماز به زبان ساده. ۲ ـ نماز ، راهنمائی آموزشی

رده بندی کنگره: ت ۲ ط/ ۱۸۶ BP

رده بندی دیویی: ۳۵۳/۲۹۷ / شماره کتابشناسی: ۳۷۸۲۴۲۶

Haki za uchapishaji zimehifadhiwa.

Chapa ya kwanza 2015

JINA LA KITABU: ..................MAFUNZO YA SAL
MUANDISHI:..........Al-Hakeem , Mohammad Saee
MCHAPAJI: ........................................ AL-WAFA
IDADI YA NAKALA : ........................................ 100
MSAMBAZAJI: ................................DARUL-HILA
ISBN: .................................................978-600-6992-27
CHAPA YA KWANZA:.................................. 2015

www.ketab.ir

# UTANGULIZI

Kila sifa njema ni stahiki ya Mwenyezi Mungu mlezi wa viumbe. Rehema na amani zimfikie mbora wa manabii na wa mwisho wa mitume, Muhammad [s.a.w.w] na kizazi chake chema kitakatifu. Na laana za Mwenyezi Mugu ziwashukie maadaui wao wote wa mwanzo mpaka wa mwisho hadi siku ya kiyama.

Ama baada…

Hakika sala ni moja ya nguzo ambazo uislamu umejengeka juu yake, si hivyo tu! Bali sala ni nguzo ya kwanza na bora zaidi baada ya imani, nayo ndio msingi wa uislamu nguzo ya dini na muhimili wake, pia [sala] ndio usia wa mwisho wa bwana mtume [s.a.w.w] pamoja na manabii, kama ambavyo ndilo jambo la kwanza atakalo ulizwa mja siku ya kiyama kama zinavyoeleza hadithi kutoka kwa mtume [s.a.w.w] na maimamu watakatifu [a.s], baadhi ya hadithi hizo zinasema: "Atakaeacha kusali kwa kusudi,Uislamu utakuwa umejitenga nae" . pia imepokelewa kua : "Utofauti kati ya ukafiri na uislamu ni kuacha sala". Na kuwa sala ndio kiunganishi baina ya mja na mola wake, na ndiyo yenye kumkumbusha mja Mola wake.

Hivyo sala ni lazima kuitilia mkazo na kuipa umuhimu na kipao mbele kama ambavyo nilazima kuwa mzingatiaji , mnyenyekevu na mtulivu wakati wa kusali, pia kuzitekeleza kwa usahihi na ukamilifu rakaa , sajida

www.ketab.ir

na matendo yake mengine, kwani iwapo sala itakubaliwa na kupokelewa ,ibada zingine nazo zitapokelewa na ikiwa haitapokelewa ibada zingine pia hazita pokelewa.

Imepokelewa hadithi kutoka kwa Imam

Sadiq [a.s] amesema: "Hakika uombezi wetu hautomfikia mwenye kupuuza sala".

Ukweli ni kua hatuwezi kuelezea yote yaliopokelewa kuhusu fadhila na ubora wa sala, bali tutatosheka na riwaya iliyopokelewa kutoka kwa Imam baqir [a.s] alisema: Amesema mtume [s.a.w.w] laiti kama mlangoni mwa nyumba ya mmoja wenu pangelikua na mto na akawa anaoga kwenye mto huo kila siku mara tano je kuna uchafu utakao baki mwilini mwake?! Nikasema hapana. Mtume akasema: Hivyo basi hakika sala ni mfano wa mto, kila mtu anaposali hufutiwa madhambi ya kati ya sala iliyopita na ya sasa.

Riwaya nyingine iliyopokelewa kutoka kwa Imam Sadiq [a.s] alisema: Sala ya faradhi [wajibu] ni bora mara ishirini zaidi ya ibada ya hija,na ibada ya hija ni bora kuliko kutoa sadaka ya dhahabu zilizojaa nyumba mpaka zikaisha.

www.ketab.ir